# Maelezo ya Haraka kuhusu Mchochota wa Ini Aina ya B

Mambo yote unayopaswa kufahamu ndani ya dakika 2!

## Mchochota wa Ini Aina ya B ni nini?

Mchochota wa Ini aina ya B ndio ugonjwa hatari zaidi wa ini ulimwenguni. Husababishwa na virusi vya mchochota wa ini aina ya B (HBV), ambayo hushambulia seli za ini na inaweza kusababisha ugonjwa wa kunyauka kwa ini (kovu), ini kushindwa kufanya kazi, au saratani ya ini.

Watu wengi wenye afya nzuri ambao wameambukizwa wakiwa watu wazima wanaweza kupambana na maambukizi na kuondoa virusi kutoka kwenye damu yao. Hii inaweza kuchukua hadi miezi 6, na wanaweza kuambukiza wakati huu. Kwa bahati mbaya, watoto wachanga na watoto wadogo wako katika hatari kubwa zaidi ya kupata maambukizi sugu (ya kudumu) wapatapo HBV.

Takribani 5-10% ya watu wazima, 30-50% ya watoto, na 90% ya watoto hawawezi kupambana na virusi na watapata maambukizi sugu. Watu walio na maambukizi sugu wanaweza kuambukiza wengine virusi (hata kama hawana dalili) na huwa katika hatari kubwa ya kupata ugonjwa wa ini na saratani ya ini baadaye maishani.

Habari njema ni kwamba mchochota wa ini aina ya B unaweza kuzuiwa kwa chanjo salama na madhubuti. Pia kuna matibabu yenye ufanisi kwa wale wanaoishi na ugonjwa sugu wa mchochota wa ini aina ya B.

## Idadi ya watu wanaogua Mchochota wa Ini Aina ya B

**Duniani:**

- Watu milioni 1.5 wataambukizwa watu milioni
- 296 duniani kote wameambukizwa ugonjwa sugu wa wa mchochota wa ini aina ya B
- Watu 820,000 hufa kila mwaka - mtu 1 kila baada ya sekunde 30 - kutokana na matatizo ya mchochota wa ini aina ya B kama vile saratani ya ini

**Marekani:**

- Angalau watu 20,000 wataambukizwa upya
- Kiasi cha Wamarekani milioni 2.4 wameambukizwa ugonjwa sugu wa hepatitis aina ya B
- Maelfu ya Wamarekani hufa kutokana na mchochota wa ini aina ya B na matatizo yake, kama vile saratani ya ini

## Je, Hepatitis B Inaweza Kuzuiwa?

NDIYO! Uliza daktari wako kuhusu chanjo salama na yenye ufanisi ya mchochota wa ini aina ya B na ujikinge mwenyewe na wapendwa wako milele. Center for Disease Control and Prevention (CDC, kituo cha Kuhibiti Magonjwa) inapendekeza kwamba watoto wote wachanga, watoto wadogo, watu wazima hadi umri wa miaka 59, na watu wazima wenye umri wa miaka 60 na zaidi ambao wako katika hatari kubwa ya kuambukizwa wapate chanjo ya mchochota wa ini aina ya B. Nje ya Marekani, World Health Organization (Shirika la Afya Ulimwenguni) linapendekeza kwamba watoto wote wachanga, wadogo, vijana waliobalehe hadi umri wa miaka 18, na watu wazima walio katika hatari kubwa kupokea chanjo hiyo. Kumbuka, unatahitaji dozi chache tu kwa ulinzi wa milele!

HEPATITIS B FOUNDATION

Hepatitis B Foundation ni shirika la kitaifa lisilo la kibiashara linalojitolea kutafuta tiba na kuboresha hali ya maisha kwa wale walioathiriwa na mchochota wa ini aina ya B duniani kote.

www.hepb.org | 215-489-4900

## Mchochota wa Ini Aina ya B Huenezwa Kwa Njia Gani?


Mchochota wa ini aina ya B huenea kupitia damu iliyoambukizwa na maji ya mwili. Hii inaweza kutokea kupitia mguso wa moja kwa moja wa damu, kushiriki ngono bila kinga, matumizi haramu ya dawa za kulevya, na kutoka kwa mwanamke aliyeambukizwa hadi kwa mtoto wake mchanga wakati wa ujauzito au kujifungua.

**Mchochota wa Ini Aina ya B unaweza kuenezwa kupitia:**

- Mgusano wa moja kwa moja na damu iliyoambukizwa
- Kushiriki ngono bila kinga
- Sindano chafu au zenye virusi (IV matumizi ya madawa ya kulevya, chale/ sindano za kutoboa)
- Kuishi katika nyumba na mtu aliyeambukizwa
- Mama aliyeambukizwa kwa mtoto wake mchanga wakati wa ujauzito au kujifungua
- Kushiriki nyembe, miswaki, vyuma vya kukata kucha, herini au vito vya mwili na mtu aliyeambukizwa
- Kuumwa na mtu aliyeambukizwa
- Vyombo visivyosafishwa vinavyotumiwa na madaktari wa meno, madaktari na vinyozi wa kando ya barabara

**Mchochota wa Ini Aina ya B hauwezi kuenezwa kupitia:**

- Kubusu shavuni au kwenye midomo
- Kukohoa au kupuna chafya
- Mgusano wa kawaida kama vile kukumbatiana, kushikana mikono au kusalimiana
- Kula chakula kilichoandaliwa au kula chakula na mtu aliyeambukizwa



## Nani yuko Hatarini Zaidi kuambukizwa Mchochota wa Ini aina ya B?

- Watoto waliozaliwa na mama walioambukizwa HBV
- Watu wanaoishi na mtu aliyeambukizwa ugonjwa sugu
- Watoto wanatunzwa na walezi kutoka katika nchi ambayo HBV imeenea
- Watu wanaoshiriki ngono bila kinga au kuwa na wapenzi zaidi ya mmoja ndani ya kipindi cha miezi 6
- Watu ambao wametambuliwa kuwa na ugonjwa wa zinaa (STD)
- Wanaume wanaoshiriki ngono na wanaume
- Watu wanaotumia sindano moja
- Wahudumu wa afya na wahudumu wa dharura
- Watu wanaosafishwa damu kupitia mshine ya figo.
- Watu wanaoishi au kufanya kazi katika mazingira ya taasisi, kama vile gereza au nyumba ya kikundi

## Nyenzo za Ziada za Hepatitis B (kwa Kiingereza)

- Hepatitis B Foundation: http://www.hepb.org
- CDC Division of Viral Hepatitis (Kitengo cha Virusi vya Mchochota wa Ini): https://www.cdc.gov/hepatitis/
- World Health Organization: http://www.who.int/mediacentre/factsheets/fs204/en/
- Immunization Action Coalition: http://www.immunize.org